

HALMASHAURI YA WILAYA YA URAMBO

(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji Wilaya)

Simu Na. 0732 988324/ 0732 988305
Fax Na. 0732 988258
Email: uramboc@yahoo.com



S. L. P. 170,
URAMBO.

Unapojibu tafadhali taja:
Kumb. Na. UDC/W.I /254/26

18/12/2017

TANGAZO LA KAZI

Halmashauri ya Wilaya ya Urambo imepokea kibali **Kumb. Na. FA.97/365/8** cha tarehe **29/11/2017** kutoka kwa **Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.** Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Urambo anawatangazia Wananchi wenyewe sifa kuomba Nafasi za kazi zilizotangazwa kama ifuatavyo:-

1. Mtendaji wa Kijiji daraja la III (Nafasi 25)

Sifa za Mwombaji:

- Awe na Elimu kidato cha Nne au sita
- Aliyehitimu mafunzo ya Cheti katika moja ya fani zifuatazo:- Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo, Dodoma au Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

Jambo la kuzingatia: Maombi yenyewe Cheti/Astashahada ya Msingi (Basic Certificate-NTA Level 4) hayatafikiriwa

Ngazi ya Mshahara: TGS B 1

Kazi na Majukumu ya kufanya:-

- Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji.
- Kusimamia Ulinzi na Usalama wa rala na mali zao, kuwa mlinzi wa Amani na Msimamizi wa Utawala Bora katika Kijiji.
- Kuratibu na kusimamia upangaji wa utekelezaji wa Mpango ya Maendeleo ya Kijiji.
- Katibu wa Mikutano yote ya Kamati za Halmashauri ya Kijiji.
- Kutafsiri na kusimamia Sera, Sheria na Taratibu.
- Kuandaa Taarifa za Utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kulekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umaskini na kuongeza uzalishaji mali.
- Kiongozi wa Wakuu wa Vitengo vya Kitaalam katika Kijiji.
- Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote za Nyaraka za Kijiji.
- Mwenyekiti wa kikao cha Wataalam walipo katika Kijiji.
- Kupokea, kusikiliza na kutatua malalamiko na migogoro ya Wananchi.
- Kusimamia utungaji wa Sheria Ndogo za Kijiji.
- Atawajibika kwa Mtendaji wa Kata.

MAELEZO YA JUMLA:-

1. Waombaji wote katika barua zao waambatanishe na maelezo binafsi (CV) .
2. Picha 2 za "**Passpot size**" ya hivi karibuni.
3. Nyaraka za vyeti zilizothibitishwa na Mamlaka za Kisheria.
4. Maombi yote yaandikwe kwa mkono.
5. Waombaji ambao ni Wafanyakazi barua zao zipitie kwa Waajiri wao wa sasa.

6. Ni muhimu kuweka namba ya simu kwa ajili ya mawasiliano.
7. Waombaji wote wawe na umri usiozidi miaka 45 na wawe Raia wa Tanzania.
8. Tarehe ya kuanza kupokea maombi ni **18/12/2017** na tarehe **ya mwisho ni 31/12/2017, saa 9.30 Alasiri.**
9. Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kughushi, wahusika watachukuliwa hatua za kisheria.

Maombi yote yatumwe kwa:-

Mkurugenzi Mtendaji Wilaya,

Halmashauri ya Wilaya,

S. L. P. 170.

URAMBO.

Makanya
Margaret J. Nakainga
MKURUGENZI MTENDAJI WILAYA
HALMASHAURI YA WILAYA
URAMBO

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
URAMBO